Innocenti Research Brief

2020-22

unicef
Office of Research-Innocenti

# UJANA SALAMA: MRADI WA NYONGEZA YA FEDHA (CASH PLUS) UNAOHUSU USTAWI NA MABADILIKO SALAMA KWA VIJANA – MATOKEO YA TATHIMINI YA KATI

## UTANGULIZI

Mradi huu wa majaribio wa 'Cash Plus' unaohusu Ustawi na Mabadiliko Salama na Yenye Afya kwa Vijana nchini Tanzania, kwa ufupi "Ujana Salama", unalenga kuimarisha maisha ya vijana wa vijijini. Vijana hawa wa umri wa balehe wanatoka katika kaya maskini na wanakabiliwa na hatari nyingi za kiafya na kiuchumi. Mradi huu unatekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (*Tanzania Social Action Fund* (TASAF)) na kuendeshwa kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (*Productive Social Safety Net* (PSSN)). Mpango huo unawalenga vijana wa umri wa balehe katika kaya zinazonufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (ruzuku inayojumuisha uhawilishaji pesa, Ujenzi au ukarabati wa miundombinu na kuimarisha njia za kujiingizia kipato katika kaya). Msaada wa kiufundi unatolewa na UNICEF Tanzania na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

Kinga ya jamii, kama vile uhawilishaji pesa, unazidi kutambuliwa kama njia muhimu ya kuwaendeleza vijana wa umri wa balehe na kuhakikisha wanakuja kuwa watu wazima wenye afya na wenye mchango katika maendeleo ya jamii. Kuwekeza katika vijana kuna matokeo bora katika kupunguza umaskini na kuleta maendeleo, hasa pale unapounganishwa na uwekezaji mwingine, kama vile katika kuendeleza miundombinu ya jamii na kutengeneza nafasi za ajira.
Mradi wa Ujana Salama unashamirishwa na ushahidi kwamba uhawilishaji fedha unaweza kuleta matokeo chanya kwa maendeleo ya vijana.[1] Hata hivyo, pesa peke yake haitoshi kumaliza matatizo lukuki yanayowakabili vijana wa umri wa balehe.[2] Utafiti wa awali unaonyesha kuwa vijana walio katika kaya zinazonufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wanakabiliwa na changamoto nyingi—kama vile kukatisha masomo, mimba za utotoni, magonjwa ya ngono, ukatili, kunyanyaswa na kuonewa—licha ya msaada wa serikali. Vilevile, ukosefu wa fursa za kiuchumi unakwamisha ukuaji salama wa vijana wa umri wa balehe kuelekea kwenye utu uzima.

Ili kukabiliana na haya, mradi wa Ujana Salama unatumia mafanikio yaliyopatikana ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini pamoja na miradi mingine, zikiwemo fursa za mafunzo na huduma ili kushughulikia




Mlengwa wa ruzuku ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, kijana na mtafiti, ukusanyaji takwimu wa kati mradi wa Ujana Salama, Halmashauri ya WIlaya Mufindi.

1 Handa, S., et al., 'The government of Kenya's cash transfer program reduces the risk of sexual debut among young people age 15-25', *PLoS One*, vol. 9, no. 1, 2014. Heinrich, C. J., Hoddinott, J. and Samson, M., 'Reducing adolescent risky behaviors in a high-risk context: The effects of unconditional cash transfers in South Africa', *Economic development and cultural change*, vol. 65, no. 4, 2017, pp. 619-652.

2 Watson, C. and Palermo, T., *Options for a "Cash Plus" Intervention to Enhance Adolescent Well-being in Tanzania: An introduction and review of the evidence from different programme models in Eastern and Southern Africa*, UNICEF, Dar es Salaam, Tanzania, 2016.

matatizo ya kipekee ya vijana wa umri wa balehe. Lengo ni kuwezesha ukuaji salama, bora na wenye tija kuelekea katika utu uzima na wakati huohuo kuimarisha uwezo wa Serikali za mitaa/vijiji kupanga, kuratibu na kusimamia huduma zinazohusiana na afya, maisha na kinga ya kijamii kwa vijana wa umri wa balehe. Uunganishwaji huu wa uhawilishaji fedha na programu za ujasiriamali , utoaji ruzuku za maendeleo na uimarishaji wa mitandao ya rufaa  na huduma ndiyo unajulikana kama muundo wa Cash Plus.

## UJANA SALAMA: MRADI WA CASH PLUS

Mradi wa Ujana Salama ulilengwa kwa vijana wa umri wa balehe wenye miaka 14–19 (katika utafiti wa mwanzo) katika kaya zinazonufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na una vipengele vikuu vitatu:

1. Mafunzo kwa vijana kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha yanayojumuisha stadi za maisha,   afya ya  uzazi na ujinsia, UKIMWI (SRH-HIV) na mbinu za kujikinga na ukatili wa kijinsia.

2. Mafunzo kwa vitendo (kuhusu njia mbadala za kuendesha maisha na kukabili matatizo) na ruzuku ya uzalishaji mali itakayotumika kwa ajili ya shule, vyuo vya ufundi, au mipango ya biashara; na,

3. Kuimarisha vituo vya afya na mtandao wa huduma rafiki kwa vijana za VVU, afya ya uzazi na ujinsia, na athari zinazotokana na vitendo vya ukatili.

Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji mawili) yalichaguliwa ili kutekeleza mradi wa Ujana Salama, hii ilitokana na kuwepo kwa Mpango  wa Kunusuru Kaya Maskini  katika maeneo hayo lakini pia UNICEF walikuwa wakisaidia programu zingine katika maeneo hayo.[3] Maeneo haya   ni katika Halmashauri nne zilizoko katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania: Hizi ni Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Mji wa Mafinga katika Mkoa wa Iringa; Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Wilaya Busokelo mkoani Mbeya. Mafunzo ya ana kwa ana kuhusu utafutaji riziki na afya ya uzazi yalitolewa katika kipindi cha majuma 12 kati ya miezi ya Februari na Mei, 2018. Wawezeshaji walikutana na vikundi vya vijana katika kila kijiji kwa saa mbili hadi nne kwa juma. Mafunzo ya utafutaji riziki na kuhusu afya ya uzazi/virusi vya UKIMWI yaliendeshwa kwa pamoja katika kila kipindi (saa moja hadi mbili kila kimoja), na kushughulikia mada zilizo kwenye Jedwali la 1.

**Jedwali la 1.** ***Mada za mafunzo***

### UJASIRIAMALI

- Ndoto na malengo
- Stadi za ujasiriamali
- Mipango ya biashara na utunzaji kumbukumbu
- Uwekaji akiba
- Wajibu wa mjasiriamali

### VVU, AFYA YA UZAZI NA UJINSIA

- Kuvuka salama kipindi cha balehe
- Mahusiano
- Elimu, kuzuia na kinga ya VVU
- Kujiweka kwenye hatari kingono na kinga
- Mimba na uzazi wa mpango
- Ukatili na ukatili wa kijinsia
- Kutatua mitazamo hasi na kaida za jinsia
- Vileo na dawa za kulevya
- kanuni za afya na lishe

Mafunzo na uangalizi wa baada ya mafunzo viliendelea kwa miezi kumi. Katika kipindi hiki, vijana wa umri wa balehe walioshiriki mafunzo na kuandaa mpango (ama wa biashara au kuendelea na elimu/mafunzo ya ufundi) walipata ruzuku ya kifedha sawa na Dola za Marekani 80 (katika mkupuo mmoja au miwili, kwa ajili ya mafunzo/ufundi au mpango wa biashara, kwa mpangilio huo).

## TATHMINI

Ili kuelewa ufanisi wa mradi huu, tathmini ya matokeo inaongozwa na Ofisi ya Utafiti ya UNICEF--Innocenti na Taasisi ya utafiti ya Economic Development Initiatives (EDI) kwa kushirikiana na TASAF, TACAIDS na UNICEF Tanzania.[4] Tathmini inatumia muundo wa Majaribio wa kuchagua sampuli kwa kutumia njia ya Bahati nasibu (RCT) katika vijiji, ambapo vijiji 130 vilichaguliwa kushiriki katika majaribio ya tafiti mbili kama ifuatavyo:

1. Kundi la vijiji linalopata afua vyenye kuleta

3 Kwa sababu za kiutawala, TASAF inagusa maeneo ya kijiografia ya utekelezaji wa programu kama Mradi wa Mamlaka ya Kieneo (PAAs). Kwa upande wa Tanzania Bara, hizi ni sawa na halmashauri za serikali za mitaa. Kisha ndani ya PAAs, haya ni kata, vijiji/mitaa (mitaa ni eneo la utawala maeneo ya mijini, sawa na vijiji huko vijijini).

4 Tathmini hii imejikita na kuchangia katika Transfer Project, ambao ni utafiti na mradi wa kujenga uelewa wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo kwa kushirikian ana Chuo Kikuu cha North Carolina huko Chapel Hill na UNICEF.

**Jedwali la 2.** ***Matokeo ya tathmini***

## MATOKEO YA MUFA MFUPI

- Hamasa za kielimu na kazi
- Mitizamo ya usawa wa kijinsia
- Uelewa wa njia za kisasa za uzazi wa mpango
- Uelewa wa njia za kuzuia VVU
- Maarifa ya kujua wapi pa kwenda kwa ajili ya huduma za afya ya uzazi/VVU na huduma za kuzuia ukatili

## MATOKEO YA KIPINDI CHA KATI HADI MUDA MREFU

- Fursa za ajira kwa vijana na miradi ya kujikimu kimaisha
- Mafanikio katika elimu na mafunzo
- Uwezo ulioongezeka wa kutafuta huduma sahihi za afya ya uzazi/VVU na huduma za mwitikio dhidi ya vitendo vya ukatili
- Kuchelewesha kuanza kushiriki ngono, ndoa na mimba za utotoni
- Kupungua kwa ukatili katika mahusiano na tabia hatarishi za VVU
- Kuimarisha afya ya akili
- Kupungua kwa kukusudia vitendo vya ukatili

suluhisho: Hii inajumuisha vijiji vilivyo kwenye mradi wa Ujana Salama vinavyopata fedha taslimu kutoka katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ikiunganishwa na mradi wa Ujana Salama;

2. Kundi la vijiji vya mlinganisho: Hii inajumjuisha vijiji vinavyopata ruzuku ya fedha pekee kutoka katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini bila nyongeza ya mradi wa Ujana Salama.

Tathmini inayoendelea inatumia njia mchanganyiko za utafiti. Tafiti zilifanyika katika vituo vya afya, kwenye jamii, kwa watoa mafunzo na vijana wa umri wa balehe katika utafiti wa mwanzo (2017), wa katikati (2018) na wa kuhitimisha 3 (2019).[5] Utafiti wa kipindi cha kati ulifanyika mara baada ya mafunzo ya ana kwa ana lakini kabla ya mafunzo kwa vitendo na ruzuku za kimaendeleo.

Tathmini zinadadisi kuhusu uelewa na hamasa zinazotarajiwa kubadilika katika muda mfupi kama matokeo ya mafunzo yanayotolewa, na pia mabadiliko ya kipindi cha kati hadi kirefu ya tabia yanayotarajiwa kutokea mara baada ya vipengele vyote vya vya Mradi wa Ujana Salamakukamilishwa.

Washiriki katika utafiti wa mwanzo walikuwa vijana wa umri wa balehe 2,458 wenye miaka 14–19. Kati yao, 2,104 walihojiwa upya katika kipindi cha kati cha utafiti (sawa na asilimia 86 ya mahojiano mapya). Matokeo ya uchambuzi wa kitakwimu yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka kwa vijana wa umri wa balehe waliohojiwa wakati wa utafiti wa mwanzo na ule wa kati – 'idadi ya washiriki'. Asilimia ya walioacha kushiriki ilikuwa sawasawa katika vijiji vya kundi linalopata afua na vile vya mlinganisho. Tabia za msingi zilibaki zilezile katika makundi yote mawili.

Kwa uchambuzi wa kitakwimu (*quantitative analysis*), tulitumia takwimu kutoka katika kundi la washiriki ambao ni vijana wa umri wa balehe katika vijiji vilivyopata afua na vile vya mlinganisho, na kulinganisha matokeo kwa kipindi fulani kati ya makundi haya mawili.[6] Kwa uchambuzi wa kimaelezo (*qualitative analysis*), tulichunguza mbinu na njia zinazoleta matokeo kupitia mahojiano ya kina na idadi ndogo ya vijana washiriki 32 wa umri wa balehe.

## MATOKEO YA UTAFITI WA KIPINDI CHA KATI

Tunaona matokeo mazuri kwa baadhi ya matokeo ya muda mfupi, yakiwemo uelewa kuhusu afya ya uzazi na VVU na mitazamo kuhusu usawa wa kijinsia. Matokeo haya yanadhihirisha jinsi vijana wa umri wa balehe, katika hatua hii ya mradi, wanavyoweza kuanza kupata maarifa mapya, na kufikiria kuhusu maisha yao ya baadaye kwa namna tofauti. Hata hivyo, hadi kipindi cha utafiti wa kati, muda wa ushiriki katika programu kwa kiasi fulani ulikuwa mfupi na baadhi ya vipengele vya mradi vilikuwa bado havijatekelezwa. Matokeo mengine ya kipindi cha kati na cha muda mrefu, kama vile mabadiliko ya tabia na kupata uzoefu, huenda yakachukua muda mrefu kutokea, jambo linaloonyesha kwa nini hatuoni mabadiliko haya katika hatua hii.

**Elimu, ushiriki katika shughuli za kiuchumi na hamasa**

5 Njia ya utafiti kwa kutumia makundi mawili tofauti ilifanyika mwaka 2017, baada ya utekelezaji wa utafiti wa mwanzo, na iligawanywa kwa PAA na vijiiji (vijiji vikubwa dhidi ya vidogo).

6 Tunatumia Uchambuzi wa ubainishaji wa Vitafitiwa Viwili Shirikishi (*Analysis of Covariance* (*ANCOVA*)), ambapo tunadhibiti takwimu za utafiti wa mwanzo kwa matokeo yaliyozingatiwa.

- Programu hii **iliongeza ushiriki wa vijana katika shughuli za kiuchumi, ikiongezewa nguvu na** ongezeko la ufugaji (kwa kaya au vijana kuanzisha shughuli zao wenyewe za kufuga). Vijana wa umri wa balehe wanaona ufugaji kama njia ya kujikusanyia utajiri ili kuwekeza katika elimu au biashara mpya baadaye. Kuongezeka kwa ushiriki katika ufugaji haukuleta matumizi zaidi ya muda katika shughuli za kiuchumi kwa ujumla.
- **Ushiriki wa vijana katika shughuli za nyumbani haukuathiriwa,** isipokuwa kutumia muda zaidi katika utafutaji na ukataji wa kuni.
- Mafunzo ya Mradi was Ujana Salama yaliendeshwa nje ya muda wa masomo, kwa hiyo **hayakuathiri mahudhurio shuleni au kusababisha vijana kukatisha masomo.**
- Programu hii haikuathiri hamasa kielimu.
- Programu iliongeza asilimia ya vijana wa umri wa balehe **wanaotaka kuwa wafanyabiashara hapo baadae.**

**Uhusiano wa VVU na SRH na huduma**

- Mradi u**likuza uelewa wa njia za kuzuia VVU** miongoni mwa wanawake lakini si kwa wanaume. Mradi uliongeza ufahamu wa wasichana kwamba kufanya ngono na mwenzi mmoja kunaweza kupunguza hatari ya VVU. Kwa ujumla, kwa vile wanaume wana ufahamu kuhusu VVU na afya ya ngono, matokeo yetu yanaonyesha kwamba mradi unawasaidia wasichana kufikia ufahamu wa wanaume.
- Takwimu nyingine za utafiti wa msingi kuhusu ufahamu wa VVU (ikiwa maambukizi ya VVU husababishwa na mbu au chakula) zilikuwa juu (zaidi ya asilimia 90) na hivyo hakukuwa na nafasi ya mabadiliko. Hakukuwa na matokeo katika viashiria hivi au kuhusu ufahamu kwamba matumizi ya mara kwa mara ya kondomu hupunguza hatari ya VVU.
- **Maarifa kuhusu njia za kisasa za kuzuia mimba yaliongezeka,** safari hii pia msukumo ukitoka kwa washiriki wanawake. Zaidi ya hayo, vijana walikuwa na uelewa mkubwa zaidi kuhusu njia za kuzuia mimba na kondomu (matokeo ya juu zaidi yalionekana kwa kwa wasichana).
- **Hakukuwa na ongezeko la idadi ya vijana wa balehe waliohitaji huduma za afya ya ngono au upimaji VVU au tiba.** Hata hivyo, miongoni mwa hao waliotafuta huduma, kulikuwa na mabadiliko katika aina ya huduma walizotafuta: Washiriki wa mradi walikuwa wakitafuta zaidi huduma za kuzuia  kuliko huduma za kutunza mimba, kulinganisha na vijana wa balehe waliokuwa katika kundi la mlinganisho.
- **Huduma za afya zimekuwa zinazowavutia zaidi vijana wa umri wa balehe,** ingawa hakukuwa na matokeo yaliyoonekana katika mada iliyojadiliwa au ubora ulioonekana wa huduma.
- **Hakuna matokeo yaliyoonekana katika uhusiano wa wenzi au tabia za ujinsia,** ikiwemo uanzishaji uhusiano; kusubiri katika kushiriki ngono na tabia baada ya kushiriki ngono mara ya kwanza; matumizi ya uzazi wa mpango; ngono kwa kubadilishana na vitu; au hatari au upimaji VVU ulioonekana.

**Usawa wa jinsia, kupunguza ukatili, afya ya akili na mitizamo**

- Mi**tazamo ya usawa wa jinsia iliongezeka miongoni mwa wanaume** (lakini si kwa wanawake), hasa kuhusu ukatili na majukumu ya nyumbani.
- Kufika utafiti wa kati, hakukuwa na **matokeo katika uzoefu wa vijana wa umri wa balehe wa ukatili wa kihisia, kimwili au kingono.**
- Hakukuwa na **matokeo kuhusu taarifa za dalili za msongo wa mawazo au au kujiona kuwa na msongo wa mawazo.**
- Hakukuwa na athari katika kuridhika na maisha, kujisikia vizuri, udhibiti wa mazingira, msukumo wa kijasiriamali au msaada ulioonekana wa kijamii.

## HITIMISHO

Mradi wa Ujana Salama unalenga kutumia matokeo ya utoaji wa ruzuku ya fedha kuwapa vijana mafunzo kuhusu kujiletea maendeleo na afya ya ngono/VVU, mafunzo kwa vitendo na utoaji ruzuku za maendeleo, na uunganishaji na huduma za afya ya ngono/VVU.

Matokeo ya utafiti wa kati yalionyesha matokeo chanya katika ufahamu kuhusu VVU na afya ya ngono, kuimarika kwa mitazamo chanya kuhusu usawa wa jinsia, na ongezeko la ari katika kuendesha biashara. Hata hivyo, vijana wa umri wa balehe wanapaswa kutafsiri kwa vitendo ari hii na maarifa mapya waliyopata. Kwa kuwa mabadiliko haya yanaweza kuchukua muda kuona matokeo halisi, tunaweza kuona athari chanya katika tabia (matumizi ya njia za uzazi wa mpango, tabia hatarishi, kwenda vituo vya afya, shughuli za kiuchumi) na uzoefu (ukatili na unyanyasaji, mimba na ndoa za utotoni) wakati wa kupitia vipengele vya mradi.

Utafiti huu unatoa mafunzo kuhusu ufanisi wa juhudi za mradi wa Ujana Salama ukitekelezwa katika miradi inayoendelea ya Kinga ya i jamii ya Serikali, na inakuza ufahamu kuhusu namna afua ya ziada kwenye Mpango kama wa Kunusuru Kaya Maskini inavyoweza kuwasaidia vijana kubadilika hadi kuwa watu wazima nchini Tanzania, Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na duniani kote.

Taarifa hii ya utafiti imeandikwa na Timu ya Tathmini ya Mradi wa Ujana Salama kwa Vijana wa Umri wa Balehe Tanzania ("Tanzania Adolescent Cash Plus Evaluation Team"). Ofisi ya Utafiti ya UNICEF—Innocenti: Valeria Groppo, Jacobus de Hoop, Lusajo Kajula, Leah Prencipe, Jennifer Waidler. Chuo Kikuu cha Buffalo: Tia Palermo (Mchunguzi Mkuu Mwenzi). EDI Global: Johanna Choumert Nkolo (Mchunguzi Mkuu Mwenzi), Respichius Mitti (Mchunguzi Mkuu Mwenzi), Nathan Sivewright, Koen Leuveld, Bhoke Munanka. TASAF: Paul Luchemba, Tumpe Lukongo. TACAIDS: Aroldia Mulokozi. UNICEF Tanzania: Ulrike Gilbert, Paul Quarles van Ufford, Rikke Le Kirkegaard, Frank Eetaama.

Ufadhili wa mradi huu wa majaribio na tathmini umetolewa na Oak Foundation na UNICEF. Fedha za nyongeza kwa ajili ya tathmini ilitolewa na DFID na Sida kupitia Ofisi ya Utafiti ya UNICEF ya misaada ya fedha—Innocenti ikisaidia Mradi wa Transfer. Fedha zaidi kwa utekelezaji wa shughuli zilitolewa na Irish Aid.

Kwa taarifa zaidi kuhusu programu na matokeo ya utafiti wa kati, soma taarifa kamili full report: Timu ya Tathmini ya Mradi wa Ujana Salama kwa Vijana wa Balehe Tanzania, Muundo wa 'Cash Plus' Kuhusu Ustawi na Mabadiliko Salama yenye Afya kwa vijana: Ripoti ya Utafiti wa Kati, Ofisi ya Utafiti ya UNICEF—Innocenti, Florence, 2020.

The Office of Research – Innocenti is UNICEF's dedicated research centre. It undertakes research on emerging or current issues in order to inform the strategic directions, policies and programmes of UNICEF and its partners, shape global debates on child rights and development, and inform the global research and policy agenda for all children, and particularly for the most vulnerable. The views expressed are those of the authors and/or editors. For rights of reproduction or translation, apply to UNICEF Office of Research – Innocenti. Short extracts may be reproduced unaltered without authorization on condition that the source is indicated. © UNICEF Office of Research

**UNICEF OFFICE OF RESEARCH-INNOCENTI**
Florence, Italy

www.unicef-irc.org

+39 055 20330

florence@unicef.org
@UNICEFInnocenti
facebook.com/UnicefInnocenti

**For every child, answers**